JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO MAALUM LA MWENGE WA UHURU JUNI 2024

www.ruvuma.go.tz

KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO MAALUM LA MWENGE WA UHURU JUNI 2024

Jarida limehariri wa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

YALIYOMO

1 Mwenge wa Uhuru mkoani Ruvuma
2.Makabidhiano ya Mwenge wa Ruvuma Ruvuma na Mtwara
3.Mwenge wa Uhuru wazindua jengo la EMD Tunduru
4.Mwenge wa Uhuru waweka jiwe la msingi mradi wa maji Tuwemacho
5.Mwenge wa Uhuru watembelea miradi 11 ya bilioni 41 Tunduru
6.Mwenge wa Uhuru wapitia miradi ya bilionin2.5 Namtumbo
7.Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kati ya Tunduru na Namtumbo
8.Hamasa ilivyokuwa mapokezi ya Mwenge Namtumbo
9.Mwenge wa Uhuru wagawa vyandarua Namtumbo
10.Mwenge wa Uhuru wagawa vifaa kwa wenye ulemavu Namtumbo
11.Mwenge wa Uhuru wapisha hodi Songea
12.Mwenge wa Uhuru waweka jiwe jiwe la msingi mradi wa maji Lipaya
13.Mwenge wa Uhuru wakagua miradi nane Mbinga Mji
14.Mwenge wa Uhuru waweka jiwe la msingi mradi sekondari ya London
15.Mwenge wa Uhuru wakagua mradi wa maji SOUWASA
16.Mwenge wa Uhuru wakagua mradi mkubwa wa barabara Songea
17.Madaba walivyoupokea Mwenge wa Uhuru

TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wanavyosikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

MWENGE WA UHURU MKOANI RUVUMA

MWENGE wa Uhuru ulianza mbio zake mkoani Ruvuma Juni 8 na kukamilisha mbio zake Juni 15,2024.

Mwenge wa Uhuru 2024,Mwenge wa Uhuru ulipokewa mkoani Ruvuma ukitokea mkoani Mtwara Juni 8,2024 katika Kijiji cha Sautimoja wilayani Tunduru.

Mwenge wa Uhuru,Juni 8 ulikimbizwa katika Halmashauri ya Tunduru,Juni 9 Namtumbo,Juni 10 Halmashauri ya Songea,Juni 11 Halmashauri ya Mbinga,Juni 12 Nyasa,Juni 13 Halmashauri ya Mbinga Mji,Juni 14 Songea Manispaa na Juni 15 Halmashauri ya Madaba.

Mwenge wa Uhuru ulikabidhiwa katika Kijiji cha Mavanga wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe Juni 16,2024.

Kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru mwaka huu ni ***tunza mazingira na shiriki uchaguzi wa serikali za mitaa kwa ujenzi wa Taifa endelevu***

MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU KATI YA MKOA WA MTWARA NA RUVUMA

Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Patrick Sawala akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed katika kijiji cha Sautimoja wilayani Tunduru.

Mwenge wa Uhuru ukiwa mkoani Ruvuma utakimbizwa katika Halmashauri zote nane za Mkoa na kuttembelea miradi 72 yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 46.

Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wwa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza baada ya kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Patrick Salawa,kulia ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Gofrey Mnzava.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas akizungumza baada ya kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Mkoa wa Mtwara

MWENGE WA UHURU WAZINDUA JENGO LA DHARURA TUNDURU

Mwenge wa Uhuru 2024 umezindua jengo la kutolea huduma za dharura (EMD)katika hospitali ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma ambapo serikali imetoa Zaidi ya shilingi milioni 369 kutekeleza mradi huo.

Akitoa taarifa ya mradi huo kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Chizza Marando amesema kati ya fedha zilizotumika shilingi milioni 300 zilitoka serikali kuu kupitia kwa wahisani (IMF) na Halmashauri ya Wilaya kupitia mapato ya ndani iliongeza Zaidi ya shilingi milioni 69.

Amesema mradi huo ulikamilika Aprili 2023 na ulianza kutoa huduma rasmi Juni 2023 ambapo hadi sasa jumla ya wateja 1,003 wamepatiwa huduma kupitia mradi huo.

“Faida za mradi huu ni Pamoja na kutoa huduma za dharura kwa wagonjwa wenye matatizo mbalimbali ya kiafya,kupunguza rufaa za matibabu kwa wagonjwa na kupunguza gharama za rufaa kwa hospitali’’,alisema Marando.

Akizungumza kabla ya kuzindua mradi huo,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Godfrey Mnzava amesema wamebaini dosari zilizojitokeza kwenye ukaguzi wa mradi huo hivyo amemuagiza Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Tunduru kufanya uchunguzi wa matumizi ya shilingi milioni 69 za nyongeza zilizotumika kwenye mradi huo bila utaratibu baada ya kuidhinishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Tunduru.

Ameongeza kuwa wamebaini baadhi ya malipo katika utekelezaji wa mradi huo yamefanyika bila vocha yake kuwa na risiti ambapo ameagiza kuwepo na uthibitisho wenye risiti za kieletroniki.

Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru umepitia na kukagua miradi 11 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.1

Kushoto ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Godfrey Mnzava alipozindua jengo la EMD katika hospitali ya Wilaya ya Tunduru

Baadhi ya wanafunzi wa sekondari ya Nakapanya wilayani Tunduru wakiwa na hamasa ya Mwenge wa Uhuru

MWENGE WA UHURU WAWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA MAJI TUWEMACHO

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge Kitaifa Godfrey Mnzava ameweka jiwe la msingi katika mradi wa maji uliopo katika Kijiji cha Tuwemacho Wilayani Tunduru Mkoani Ruvuma mradi ambao unatekelezwa kwa kiasi cha sh. Bilioni 1,054,232,603.55 na mpaka sasa kiasi cha sh. 138,134,890.00 zimetumika kumlipa mkandarasi.

Mradi huo ambao unatekelezwa na wakala wa maji na usafi wa mazingira vijijini (RUWASA) umesanifiwa kuhudumia wananchi wapatao 3527 katika Kijiji cha Tuwemacho.

Awali akiweka jiwe la msingi mradi huo kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa Godfrey Mnzava alisema kuwa ameridhishwa na mradi huo baada ya kukagua miundombinu, Nyaraka na kuangalia usimamizi ulikuwaje hivyo Mwenge wa Uhuru umejiridhisha na usimamizi wote uliofanyika kwenye mradi huo pasipo na shaka yoyote.

" Nitoe angalizo kwa wananchi ambao tunapata huduma hii muhimu ya maji, tuwe makini kutunza miundombinu hii, tuwe makini kutunza vyanzo vya maji na mabomba ambayo yanatupatia huduma hii muhimu sisi sote tunajuwa kwamba maji ni huduma muhimu sana na uwepo wa maji unaleta faraja kubwa sana kama tunavyoona akina mama wanashangilia kwa kuwa mradi huu umetakuwa na manufaa makubwa" alisema Mnzava.

Akisoma taarifa Taarifa ya mradi huo kwa kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa Injinia Maua Mgallah alisema kuwa mradi huo wa maji ulianza January 5/2024 na kutarajiwa kukamilika Julai 4 mwaka huu.

Alisema kuwa lengo la mradi huo ni kupunguza ama kuondoa kabisa tatizo la ukosefu wa huduma ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

MWENGE WA UHURU WATEMBELEA MIRADI 11 YA BILIONI 4.1 TUNDURU

Mwenge wa Uhuru umetembelea miradi 11 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.1 katika Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Mheshimiwa Peres Magiri amesema Mwenge huo umekimbizwa umbali wa kilometa 284 na kwamba ukiwa kwenye mkesha wilayani humo wananchi walijitokeza kupima afya zao.

Amesema jumla ya watu 173 walijitokeza kupima Virusi vya UKIMWI(VVU) na hakuna hata mtu mmoja aliyepatikana na maambukizi ya VVU na wananchi pia walijitokeza kuchangia damu kwa hiari.

Moja ya miradi iliyozinduliwa na Mwenge wa Uhuru wilayani Tunduru ni mradi wa ujenzi wa jengo la kutolea huduma za dharura (EMD) katika hospitali ya wilaya ya Tunduru ambapo serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 369 kutekeleza mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo amesema mradi huo umekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi ambapo hadi sasa jumla ya wateja 1,003 wamepatiwa huduma kupitia mradi huo.

Mradi mwingine ambao umepitiwa na Mwenge wa Uhuru wilayani Tunduru ni ujenzi wa mradi wa maji safi katika Kijiji cha Tuwemacho ambapo serikali imetoa Zaidi ya shilingi bilioni moja kutekeleza mradi huo.

Meneja wa RUWASA wilayani Tunduru Mhandisi Maua Mgallah amesema mradi huo ukikamilika utawanufaisha wananchi wapatao 3,527 hivyo kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama.

Akizungumza baada ya kukagua mradi wa maji,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Godfrey Mnzava ameridhishwa na utekelezaji wa mradi huo wa maji ambao amesema utapunguza changamoto ya wananchi kutembea umbali mrefu kufuata maji.

Miradi mingine iliyotembelewa na Mwenge wa Uhuru wilayani Tunduru ni mradi wa ugawaji wa vyandarua kwa akinamama wajawazito na Watoto ambao umewezesha wagonjwa wa malaria kupungua kutoka 99,469 mwaka 2021/2022 hadi wagonjwa 88,730 mwaka 2022/2023.

Mwenge wa Uhuru pia umetembelea mradi wa lishe,mradi wa ugawaji vifaa kwa makundi yenye mahitaji maalum na mradi wa ujenzi wa nyumba ya walimu ya familia mbili katika sekondari ya Kungu iliyojengwa kwa gharama ya shilingi milioni 95.

Mradi mwingine ni wa kituo cha malezi ya vijana cha kilimo na mifugo la Kanisa la Upendo wa Kristo KIUMA ambapo mradi huo umegharimu Zaidi ya shilingi bilioni1.5,gharama zinazohusisha majengo, vitalu,nyumba,visima vya maji ya kumwagilia na mashine zake,bustani na mifugo.

Baadhi ya wakimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa wakionesha kwa vitendo kukimbiza Mwenge wa Uhuru

MWENGE WA UHURU WAPITIA MIRADI YA BILIONI 2.5 NAMTUMBO

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngolo Malenya amesema kuwa Mwenge wa Uhuru katika Wilaya hiyo umefungua,kuweka mawe ya msingi na kuzindua miradi kumi ya maendeleo yenye thamani ya sh. bilioni 2.5

Malenya ameitaja miongoni mwa miradi hiyo kuwa ni mradi wa ujenzi wa barabara za lami mjini Namtumbo ambao unagharimu Zaidi ya shilingi milioni 889,mradi ambao unahusisha ujenzi wa wa barabara kwa kiwango cha changarawe,lami nyepesi,kokoto na uwekaji taa za barabarani 43.

Mradi mwingine ambao umepitiwa na Mwenge wa Uhuru ni ujenzi wa mabweni katika chuo cha Ufundi Stadi VETA Namtumbo,mradi ambao unatarajia kugharimu Zaidi ya shilingi milioni 814.

Mwenge wa Uhuru pia umepitia miradi ya lishe na shamba la miti katika Kijiji cha Luegu ambapo hadi kufikia mwaka 2023 shamba hilo lilikuwa na miti 5480 aina ya mitiki na kwamba mradi huo umegharimu shilingi milioni 45.

Mwenge wa Uhuru pia umepitia mradi wa chemchem ya maji ya asili iliyoboreshwa katika Kijiji cha Ruvuma Kata ya Hanga ambapo Zaidi ya shilingi milioni mbili zimetumika kuboresha chemchem hiyo.

Miradi mingine iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru wilayani Namtumbo ni kituo cha mafuta cha KSM kilichoanzishwa na Said Kazibure ambapo hadi sasa mradi umegharimu shilingi milioni 515 na kwamba mradi unatarajia kutoa ajira 25.

Mwenge wa Uhuru umepokea taarifa ya ugawaji wa vyandarua kwa akinamama wajawazito,makundi maalum na Watoto chini ya mwaka mmoja,pia Mwenge wa uhuru umepokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za ukatili wa kijinsia na watu wenye ulemavu.

Akizungumza baada ya kukagua mradi wa barabara za lami mjini Namtumbo,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Godref Mnzava ameipongeza TARURA kwa usimamizi mzuri wa mradi huo ambao pia umezingatia mfumo wa ununuzi wa umma katika utekelezaji wake.

Amesema serikali inaendelea kuelekeza manunuzi yote na zabuni zake yapite kwenye mfumo wa manunuzi wa kidigitali wa NEST ambapo amewapongeza TARURA kwa kutekeleza agizo hilo kwa kupitisha zabuni kwenye mfumo hivyo kuongeza uwazi na uwajibikaji.

MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU KATI YA WILAYA YA TUNDURU NA NAMTUMBO

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngolo Malenya amesema kuwa Mwenge wa Uhuru unaokimbizwa katika Wilaya hiyo utakagua,utaweka mawe ya msingi na kuzindua miradi kumi ya maendeleo yenye thamani ya sh. Bilioni 2.5

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kutoka Wilaya ya Tunduru alisema kuwa mwenge huo ukiwa Wilayani Namtumbo utaweka jiwe la msingi kwenye mradi wa barabara ,Mradi wa kituo cha mafuta,mradi wa bweni Veta, ugawaji wa vifaa kwa watu wenye mahitaji maalumu.

Ameitaja miradi mingine kukagua shughuli za lishe, kuzindua klabu ya kupinga Rushwa, kutembelea mradi wa uhifadhi wa mazingira Luegu, pamoja na kuzindua kisima kilichoboreshwa Kijiji Ruvuma.

KIONGOZI MWENGE WA UHURU AGAWA VYANDARUA NAMTUMBO

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Godfrey Mnzava akigawa vyandarua kwa akinamama wa kijiji cha Mchomoro Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ambapo Mwenge wa Uhuru ulitembelea miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.5

Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru katika Kijiji cha Mchomoro wilayani Namtumbo

HAMASA ILIVYOKUWA MAPOKEZI YA MWENGE NAMTUMBO

VIJANA wa hamasa kwenye mapokezi ya Mwenge wa Uhuru wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma hapa ni kijiji cha Mchomoro ambako yalifanyika makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo

MWENGE WA UHURU WAKABIDHI VIFAA VYA WENYE ULEMAVU NAMTUMBO

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Gofrey Mnzava amekabidhwi vifaa kwa watoto wenye mahitaji maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ambapo amesema serikali ya Awamu ya Sita inawathamini watu wenye ulemavu ndiyo maana inajitahidi kupunguza changamoto mbalimbali zinazowakabili

Kulia ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Gofrey Mnzava akikagua mradi wa barabara za lami mjini Namtumbo,katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mhe.Ngollo Malenya

MWENGE WA UHURU ULIVYOBISHA HODI WILAYANI SONGEA

Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Mheshimiwa Ngollo Malenya akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile.Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri hiyo imekagua miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.5

MIRADI YA MWENGE WA BILIONI 4.5 YATEMBELEWA NA MWENGE WA UHURU SONGEA

Mwenge wa Uhuru 2024 umetembelea miradi 10 ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.5 katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa maji mtiririko katika Kijiji cha Lipaya Kata ya Mpitimbi,Meneja wa RUWASA Wilaya ya Songea amesema mradi wa maji Lipaya ni miongoni mwa miradi ya maji mitatu inayojumuisha vijiji vya Lipaya,Kizuka na Lipokela.

Amesema miradi hiyo inatekelezwa kwa kwa gharama ya shilingi bilioni 3.4 iliyopangwa kuhudumia wananchi wapatao 10,394 ambapo amesema katika mradi wa maji Lipaya wenye thamani ya shilingi bilioni 1.9 utahudumia wananchi wapatao 3,886.

Kwa mujibu wa Meneja huyo wa RUWASA mradi wa maji Kizuka unagharimu Zaidi ya shilingi milioni 730 na mradi wa maji Lipokela unagharimu Zaidi ya shilingi milioni 734 na kwamba miradi hiyo itasogeza huduma za maji safi na salama Jirani na wananchi.

Mwenge wa Uhuru pia umeweka jiwe la msingi katika mradi wa jengo la dharura katika hospitali ya misheni ya Mtakatifu Joseph Peramiho ambapo hadi sasa Zaidi ya shilingi milioni 896 zimetumika kutekeleza mradi huo ambao unatarajia kutumia Zaidi ya shilingi bilioni 1.5 hadi kukamilika.

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea pia umefungua bweni katika shule ya sekondari ya Jenista Mhagama ambapo serikali

imetoa shilingi milioni 128 kujenga bweni hilo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80.

Mradi mwingine ambao umewekwa jiwe la msingi na Mwenge wa Uhuru ni mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa katika Kijiji cha Lundusi Peramiho ambapo serikali imetoa Zaidi ya shilingi milioni 434 kutekeleza mradi huo ambao unahusisha ujenzi wa stendi,maduka 36,vyoo matundu nane,jengo la utawala na vibanda viwili vya walinzi.

WANANCHI wa kijiji cha Lipaya Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma wakiungana va wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa kukimbiza Mwenge wa Uhuru kutoka eneo la makabidhiano ya Wilaya ya Namtumbo na Songea hadi kwenye mradi wa maji wa RUWASA .

Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa wakiwa kwenye banda la lishe Halmashauri ya Songea

MWENGE WA UHURU WAWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA MAJI LIPAYA

Mwenge wa Uhuru 2024 umeweka jiwe la msingi katika mradi wa maji ya mtiririko katika kijiji cha Lipaya Kata ya Mpitimbi Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma ambapo serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 3.4 kutekeleza mradi huo ambao unatekelezwa katika vijiji vya Lipaya,Lipole na Kizuka ambapo mradi unatarajia kuhudumia wananchi wapatao 10,394 kutoka katika vijiji hivyo.

Hata hivyo katika kijiji cha Lipaya mradi huo unagharimu shilingi bilioni 1.9 na unatarajia kuhudumia wananchi wapatao 3,886,ambapo katika kijiji cha Lizuka mradi unagharimu zaidi ya shilingi milioni 730 na katika katika kijiji cha Lipokela Mwenge wa Uhuru unatarajia kugharimu zaidi ya shilingi milioni 734.

Mwenge wa Uhuru umeridhia kuweka jiwe la msingi katika mradi huo.

MWENGE WA UHURU WAIKUBALI MIRADI YOTE MBINGA

Mwenge wa Uhuru 2024 umeikubali miradi yote yenye thamani ya Zaidi ya shilingi bilioni moja iliyoipitia katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Akizungumza kwenye makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kati ya Halmashauri ya wilaya ya Songea na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga,Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Mheshimiwa Kisare Makori amesema Mwenge huo katika Halmashauri hiyo umekimbizwa jumla ya kilometa 110.9 na kutembelea miradi sita yenye thamani ya shilingi bilioni 1.1.

Akitoa taarifa ya ufunguzi wa mradi wa kituo cha Afya Litumbandyosi kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Joseph Rwiza amesema hadi sasa Zaidi ya shilingi milioni 824 zimetumika kujenga kituo hicho ambacho kinahudumia wakazi 11,506 wa Kata ya Litumbandyosi.

Ametaja lengo la kujenga kituo hicho ni kusogeza huduma za afya kwa wananchi ili kupunguza gharama za matibabu kwa wakazi wa Kata hiyo yenye vijiji vinne vya Mabuni,Luhagara,Kingoli na Litumbandyosi.

Mradi mwingine uliopitiwa na Mwenge wa Uhuru ni shamba la miti ya mitiki lililopo katika Kijiji cha Mabuni lenye jumla ya miti 2,692 linalomilikiwa na Festo Mhagama.

Mwenge wa uhuru pia umetembelea chanzo cha chemchem ya Mto Askofu uliopo katika Kijiji cha Paradiso Kata ya Ruanda ambapo Chemchem hiyo ina uwezo wa kuzalisha maji wastani wa lita 16,000 kwa siku na ipo katika hifadhi ya msitu wa Kijiji cha Paradiso chenye wakazi wapatao 2,766.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Godrey Mnzava ameridhia kuzindua mradi wa madarasa mawili katika shule ya sekondari Ruanda ambayo yamegharimu Zaidi ya shilingi milioni 48.

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga pia umekagua kikundi cha wanawake kinachoitwa Umoja wa Wanawake Mbalawala ambacho kinaendesha mradi wa utengenezaji na uuzaji wa nishati ya makaa ya mawe ya kupikia ambapo jumla ya shilingi milioni 130 zimetumika kutekeleza mradi huo

MIRADI YOTE SABA YAPITISHWA NA MWENGE WA UHURU NYASA

MBIO za Mwenge wa Uhuru 2024 zimeikubali miradi yote saba yenye thamani ya shilingi bilioni 4.4 iliyoipitia katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

Akitoa taarifa ya mradi wa maji wa Ngumbo kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Godfrey Mnzava,Meneja wa RUWASA Wilaya ya Nyasa Mhandisi Masoud Samila amesema mradi huo unagharimu Zaidi ya shilingi bilioni 2.5 na utekelezaji wake umefikia asilimia 100.

“Mradi unawanufaisha wananchi 11,080 waliopo katika vijiji sita vilivyopo katika kata za Ngumbo na Liwundi na mradi umepunguza umbali mrefu wa wananchi kutafuta huduma ya maji’’,alisema.

Mradi mwingine ambao umezinduliwa na Mwenge wa Uhuru 2024 ni mradi wa ujenzi wa barabara ya lami katika Mji wa Mbambabay,mradi huo ambao

umekamilika kwa asilimia 100 umegharimu shilingi milioni 500 kujenga lami nyepesi yenye urefu wa kilometa 0.88.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Nyasa Mhandisi Thomas Kitusi amezitaja faida za mradi huo kuwa ni Pamoja na kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara,kupunguza athari za kimazingira kwenye maeneo yanayochukuliwa changarawe na kuongeza mtandao wa barabara za lami katika Wilaya ya Nyasa kutoka kilometa nne hadi 5.1.

Mwenge wa Uhuru pia umeweka jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari Lovund inayojengwa katika Kata ya Kilosa Mbambabay ambapo hadi sasa mradi umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 703 na unatarajia kutumia Zaidi ya shilingi bilioni 1,2 hadi kukamilika.

Mratibu wa Mradi huo Denis Katumbi ameitaja miundombinu iliyojengwa kuwa ni vyumba nane vya madarasa,nyumba tatu za walimu,nyumba ya Mkuu wa shule,jengo la utawala,maabara tatu,matundu ya vyoo 17,maktaba,bwalo la chakula,uzio kuzunguka eneo la shule,taki la maji la lita 5,000 na kichomea taka.

Mwenge wa Uhuru pia umetembelea mradi wa uhifadhi wa mistu wa asili wa Namswea wenye ukubwa wa keta 23,046, ambao umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 42.

Msitu wa Namswea unaunganisha kata nne ambazo ni Linga,Lituhi,Mbaha na Ngumbo na utekelezaji wa uhifadhi wa msitu huo umezingatia sera ya mpango shirikishi wa usimamizi wa misitu ambapo vijiji 11 vimeungabishwa kupitia Kamati za Maliasili za vijiji.

MWENGE WA UHURU WAKAGUA MIRADI NANE MBINGA MJI

MWENGE wa Uhuru umeendelea na mbio zake mkoani Ruvuma kwa kupitia miradi nane yenye thamani ya shilingi bilioni 2.1 katika Halmashauri ya Mji Mbinga.

Mwenge wa Uhuru ukiwa mjini Mbinga umekagua mradi wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje,jengo la maabara na jengo la upasuaji katika hospitali ya Halmashauri ya Mbinga,mradi ambao unatekelezwa kwa gharama ya Zaidi ya shilingi milioni 900.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo amesema mradi huo ukikamilika utaongeza miundombonu toshelezi kwa watoa huduma na wagonjwa,kupanua wigo kwa watoa huduma za afya kwa makundi maalum na kuanzishwa huduma mpya za kuchunguzi.

Hata hivyo licha ya kuweka jiwe la msingi kwenye mradi huo,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Godfrey Mnzava ameiagiza TAKUKURU kufanya uchunguzi wa kina kwenye mradi huo,baada ya mwenge wa Uhuru kubaini utekelezaji wa mradi huo haukufanyika kupitia mfumo wa manunuzi ya umma wa NeST kama ilivyoelekezwa na serikali.

Mwenge wa Uhuru ukiwa mjini Mbinga umekagua mradi wa kuboresha huduma ya maji safi katika Kijiji cha Utiri na kuweka jiwe la msingi,mradi ambao unagharimu Zaidi ya shilingi milioni 421.

Mradi wa uboreshaji huduma ya maji safi Utiri unahudumia wakazi wapatao 3,857 ambapo lengo la mradi ni kusogeza huduma ya maji ili kuwapunguzia wananchi kero ya kutembea kutafuta maji.

Mradi mwingine ambao umefunguliwa na Mwenge wa Uhuru mjini Mbinga ni ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya msingi Myangayanga ambao umegharimu shilingi milioni 48.

Mwenge wa uhuru umeweka jiwe la kutembelea kiwanda cha kukoboa kahawa Mbinga ,mradi ambao umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 725.

Akizungumza kwenye kiwanda hicho,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Godfrey Mnzava amesema licha ya kiwanda hicho kuwa na manufaa kiuchumi ikiwemo kutoa ajira za kudumu 76 na za muda 300,ameuagiza uongozi kuwanunulia vifaa vya usalama kazini wafanyakazi wote wa kiwanda hicho.

Mwenge wa Uhuru mjini Mbinga umekagua mradi wa shamba la mbegu bora za miti katika Kijiji cha Utiri lenye ukubwa wa ekari 23.8 linalomilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Mbinga na kuendeshwa kwa ubia kati ya Halmashauri ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kwa ufadhili wa Ubalozi wa Finland.

Mradi huo umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 55 na kwamba lengo la mradi ni kuzalisha mbegu bora za miti ambazo zinapatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Mwenge wa Uhuru ukiwa mjini Mbinga pia umepokea taarifa ya mapambano dhidi ya malaria ambapo Halmashauri imenunua vyandarua 43,955 vyenye thamani ya Zaidi ya shilingi milioni 404 ambavyo vimegawiwa bure kwa wajawazito, ,Watoto na wanafunzi ili kufikia adhima ya serikali ya Ziro Malaria ifikapo mwaka 2023.

Mwenge wa Uhuru ulipokagua mradi wa ujenzi majengo matatu hospitali ya Mji wa Mbinga

MWENGE WA UHURU WAWEKA JIWE LA MSINGI SEKONDARI YA LONDONI SONGEA

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 ameweka jiwe la msingi ujenzi wa vyumba kumi vya madarasa na matundu kumi ya vyoo vinavyogharimu zaidi ya shilingi milioni 256 katika shule ya sekondari Londoni Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma

Shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2004 ina wanafunzi wanaosoma kidato cha kwanza hadi cha sita wapatao 1,399

MWENGE WA UHURU WAKAGUA MRADI WA MAJI SOUWASA

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Manispaa ya Songea umetembelea mradi wa maji Mtaa wa Pambazuko Kata ya Tanga unaogharimu Zaidi ya shilingi milioni 578 wenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapata0 15,990.Mradi huo unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Ustawi wa Mazingira Songea (SOUWASA) kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira.

MWENGE WA UHURU WATEMBELEA MRADI MKUBWA WA BARABARA SONGEA

Mwenge wa Uhuru 2024 umetembelea mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara za lami nzito zinazogharimu Zaidi ya shilingi bilioni 22 katika mji wa Songea mkoani Ruvuma.

Akitoa taarifa ya mradi huo kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Wakili Bashir Muhoja amesema Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni miongoni mwa Halmashauri 12 zilizobahatika kupata mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya barabara za lami nzito zenye urefu wa kilometa 10.1.

Amebainisha mradi huo una jumla ya barabara 20 za lami katikati ya Mji wa Songea ambazo zitatengezwa kupitia mradi huo ambao umefadhiliwa na Jumjuiya ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA) kupitia Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha miundombinu na ushindani wa miji,Manispaa na Majiji nchini Tanzania (TACTC).

Hata hivyo amebainisha kuwa mradi huo unaratibiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI na kwamba hadi sasa Mkandarasi amefikia asilimia 20 ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara hiyo.

“Ujenzi wa barabara hizi utaleeta manufaa ya kuwa na miundombinu bora na inayopitika wakati wote

hivyo kuwezesha watumiaji wa barabara kupunguza gharama za uendeshaji wa vifaa vya moto,kutoa ajira kwa wananchi 134 na kuimarisha ulinzi na usalama kwa kuwa barabara hizo zitakuwa na taa’’,alisisitiza.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Godfrey Mnzava ameagiza Mkandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo ili uanze kuwahudumia wananchi wa Mji wa Songea.

Mwenge wa Uhuru pia umeweka jiwe la msingi la ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea ambao unatekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 500.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Godfrey Mnzava pia amekubali kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa vyumba kumi na matundu kumi katika shule ya sekondari ta Londoni Manispaa ya Songea,mradi ambao unagharimu Zaidi ya shilingi milioni 259.

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Manispaa ya Songea umetembelea mradi wa maji Mtaa wa Pambazuko Kata ya Tanga unaogharimu Zaidi ya shilingi milioni 578 wenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapata0 15,990.

MWENGE WA UHURU ULIVYOPOKEWA HALMASHAURI YA MADABA

Mwenge wa Uhuru 2024 umehitimisha mbio zake mkoani Ruvuma kwa kukagua miradi katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea.

Akitoa taarifa kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa 2024 kuhusu mradi wa ujenzi wa maji katika Kijiji cha Mbangamawe Halmashauri ya Madaba,Meneja wa RUWASA Wilaya ya Songea Mhandisi Mathias Charles amesema RUWASA ilipokea Zaidi ya shilingi milioni 545 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji hicho.

Amesema utekelezaji wa mradi huo umehusisha ujenzi wa tanki lenye uja zo wa lita 50,000,ujenzi wa banio la maji,ujenzi wa sampu tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 30,000,nyumba ya mtambo,chumba cha mlinzi,choo na vituo sita vya kuchotea maji .

Amesema mradi huo una faida mbalimbali zikiwemo wananchi wapatao 2,800 kunufaika na upatikanaji wa huduma ya maji na salama hivyo kupunguza umbali wa kufuata maji.

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Madaba umeweka jiwe la msingi ujenzi mradi wa lami nyepesi barabara ya Kifaguro-Magingo yenye urefu wa kilometa 5.6

Mradi huo unatekelezwa na TARURA kwa gharama ya Zaidi ya shilingi milioni 563 ambapo kukamilika kwa ujenzi wa mradi huo,kutarahisisha wananchi wa Halmashauri hiyo kufika kwa urahisi katika jengo la Makao makuu ya Halmashauri, hospitali ya Wilaya,shule ya msingi Kifaguro na sekondari ya Madaba hivyo kupata huduma za kijamii kwa urahisi.

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Madaba pia umekagua mradi wa upandaji miti katika uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji hifadhi ya Wino ambayo ina ukubwa wa hekta 39,718,Msitu huo unaoundwa na safu tatu za Wino,Ifinga na Mkongotema.

Hifadhi ya Msitu wa Wino inaendelea na uhifadhi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji na kuvitumia katika shughuli za uzalishaji wa miche ya kupanda na matumizi ya majumbani.

Miongoni mwa vyanzo vya maji muhimu vinavyoendelea kulindwa ni Igawisenga, Mgombezi, Mwendesi na Kibanditi ambapo wananchi wamepanda miti 20,000 itakayosaidia kutunza vyanzo vya maji,kuimarisha kilimo cha zao la nyuki na kupanda matunda mbalimbali.

Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Madaba umeweka jiwe la msingi la ujenzi wa soko la Lituta linalogharimu Zaidi ya shilingi milioni 190 na kwamba kukamilika kwa mradi huo kutaongeza mapato katika Kijiji na kuboreshwa mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Godfrey Mnzava amekagua na kuzindua vyumba viwili vya madarasa na matundu matatu ya vyoo katika shule ya msingi Ngadinda ambapo jumla ya shilingi milioni 53 zimetumika kutekeleza mradi huo.

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Madaba ulisomewa taarifa ya ugawaji wa vyandarua kwa akinamama wajawazito na Watoto chini ya mwaka mmoja ambapo katika kipindi cha Julai 2023 had Mei 2024 Halmashauri hiyo ilipokea vyandarua 5040 vyenye thamani ya Zaidi ya shilingi milioni 36

RUVUMA YAUKABIDHI MWENGE WA UHURU NJOMBE

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge akizungumza baada ya kumkabidhi Mwenge wa Uhuru Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe Judica omari katika kijiji cha Mavanga wilayani Ludewa .

Makatibu Tawala hao wa mikoa wamefanya makabidhiano hayo kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Ruvuma na Njombe

Mwenge wa Uhuru ulianza mbio zake mkoani Ruvuma Juni 8 na kukamilisha Juni 15 mwaka huu .

Ukiwa mkoani Ruvuma mwenge wa Uhuru umetembelea miradi 72 yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 46 iliyopo katika Halmashauri zote nane za Mkoa huo .

HABARI PICHA MWENGE WA UHURU 2024

Mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa katika Kijiji cha Ngumbo wilayani Nyasa mkoani Ruvuma ambao serikali imetoa shilingi bilioni 2.5 kutekeleza mradi huo unaozinufaisha kata za Ngumbo na Liwundi

JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA

Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

S.L.P 74 SONGEA

57180 RUVUMA
SIMU Nambari.025- 2602256/2602238
FAX Na.2602144
E-MAIL: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
TOVUTI:www.ruvuma.go.tz
INSTAGRAM; rs ruvuma
FACEBOOK: rs ruvuma
YOUTUBE:rs ruvuma